
KISWAHILI - CBC GRADE 1 TERM 2 2022

MASWALI

1. **ZOEZI 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**
   Jibu maswali haya utakayoulizwa na mwalimu wako. (Alama 5)
   a. Taja vifaa viwili vya darasani.
   b. Jibu salamu: Shikamoo?
   c. Taja sehemu mbili za mwili.
   d. Tambua vifaa vitatu ya usafi.
   e. Neno "babu' lina herufi ngapi?
2. **ZOEZI LA 2: KUSOMA KWA SAUTI**
   Soma kifungu hiki kwa sauti.
   Mimi ni Abdi. Rafiki yangu anaitwa Musa. Siku ya Jumamosi, sisi hucheza pamoja. Leo tunacheza mchezo na Kibe. Musa kufumba macho yake asinione. Mimi ninakimbia ili nijifiche. Nimejificha nyuma ya kiti. Nimejifunika kichwa kwa kitambaa. Musa hajaniona.
3. **ZOEZI LA 3: SARUFI**
   Andika majina ya picha zifuatazo. (Alama 3)



4. Andika nambari kwa maneno. (Alama 4)
   a. 6
   b. 3
   c. 4
   d. 1
5. Jibu maamkuzi yafuatayo. (Alama 5)
   a. Shikamoo?
   b. U hali gani?
   c. Habari?
   d. Hujambo?